

## 11D-Makhaarij Al-Huruwf (Matokeo Ya Herufi) - Ash-Shafataan (Midomo Miwili)

### 4.- الشَّفَاتَان Ash-Shafataan - Midomo miwili:

Kunapatikana makhraj mbili inayotoa herufi nne:

- i) Kutoka katika tumbo la mdomo wa chini na meno ya mbele ya juu inatoka herufi ya ف
- ii) Midomo miwili yote inapofungwa; pamoja na kushirikishwa na pua (khayshuwm) inatoka herufi ya م .  
Midomo miwili yote inapofungwa mfungo wa nguvu hutoka herufi ya ب.

Herufi ya و isiyokuwa ya madd inatoka kwa kukusanyika midomo yote miwili mbele pamoja na kubakia uwazi wenye kutoka sauti ndani yake.